



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI  
ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KAHAMA



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KIFO CHA BI. RACHAL WILLIAM ZEPHANIA**

Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama inakiri kutokea kwa kifo cha Mtajwa hapo juu kilichotokea Siku ya Tarehe 28/12/2023 kwenye Hospitali ya Manispaa ya Kahama.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Mstahiki Meya Kwa niaba ya Baraza la Madiwani na Mbunge wa Jimbo la Kahama wanatoa pole kwa Wafiwa na wote walioguswa na Msiba wa mpendwa wao.

Taarifa za awali zinaonesha kuwa kulikua na uzembe wa baadhi ya watoa huduma za Afya waliokuwa zamu usiku wa tarehe 27/12/2023 kulikopelekea kifo cha Bi. Rachal William Zephania

Tunapenda kuutarifu umma kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama imeshachukua hatua za kinidhamu kwa Kuwasimamisha Kazi Watumishi Sita (6) ili kupisha uchunguzi.

Watumishi waliosimamishwa kazi ni:

1. Dkt. Christina Renatus Kulwa – Daktari Daraja la II
2. Bi Joyce Kwangu Shindayi – Afisa Mteknolojia Maabara Daraja la I
3. Bi. Silya Sayenda Kuchibanda – Afisa Muuguzi Msaidizi Daraja la I
4. Bi. Betina Gozbert Lwamuzigu - Afisa Muuguzi Msaidizi Daraja la I
5. Nuru Philip Mwahayonga- Afisa Muuguzi Msaidizi Daraja la II
6. Bi. Lemi Majige Mwanzalima – Muuguzi Daraja la I

Aidha imeundwa timu ya Uchunguzi na Mkuu wa Wilaya ya Kahama kwajili ya kufuatilia hatua kwa hatua dhidi ya tukio hilo.

Mkurugenzi wa Halmashauri anawaasa Watumishi wote kufanyakazi kwa Mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu katika Utumishi wa Umma.

C. B. Mkusa

**KAIMU MKURUGENZI**  
**HALMASHAURI YA MANISPAA**

**KAHAMA**

**02 Januari, 2024**

**MUNICIPAL DIRECTOR**  
**KAHAMA MUNICIPAL COUNCIL**  
**P.O. Box 472**  
**KAHAMA**